**15** Wanawake wanaoishi kwenye umaskini na hawawezi kusoma wala kuandika wapate fursa ya kujifunza neno la Mungu kupitia redioni. Ombea upatikanaji wa vipindi vya wanawake wa matumaini kupatikana kwa lugha nyingi zaidi.

**16** Wanawake wanaoteseka kutokana na mazoea ya ndoa za wake wengi. Omba ili sheria nyingi zitungwe na kuimarishwa ili kulinda taasisi ya familia.

**17** Wazazi kutoa elimu kwa watoto wao wa kike na sio kuwalazimishwa kuolewa ili wapate mahari kutokana na ugumu wa kifedha kwenye familia. Ombea wasichana waelewe vizurihaki zao na kukataa kulazimishwa kuolewa na kwamba voingozi wa kijamii watoe ulinzi kwa wasichana hawa.

**18** Maelfu ya watoto wanaofanya kazi kwenye mashimo chini sana migodini kusikokuwa salama na wanakaa zamu za masaa 24; pia wakumbuke wanaosafirisha na kupasua mizigo mikubwa ya dhahabu. Hii inaweka hatarini kutokana na kuporomoka ngema na madhara ya kiafya kutokana na zebaki, kuvuta pumzi yenye vumbi na kubeba mizigo mizito. *(http://allafrica.com/stories/201507011641.html)*. Takriban wato asilimia 70 ya watu milioni 50 Tanzania wanaishi kwenye umaskini mkubwa.

**19** Egide (Mkurugenzi wa TWR Afrika Mashariki), Rachel (Mkurugenzi wa TWR Burundi), Beatrice (mratibu wa Project Hannah), Consolata (mratibu wa maombi), na Gervais (mtafsiri wa kalenda ya maombi kwa Kirundi). Ombea utafsiri wa vipindi vya Wanawake wa matumaini na fedha zinazohitajika ili kuvirusha redioni.

**20** Viongozi wa Afrika mashariki watoe maji safi ya kunywa yanayohitajika sana na vifaa vya usafi ili kuzuia magonjwa yanayoua yanayochukua mamilioni ya watu kila mwaka.

**21** Waombaji wa Project Hannah kwenye makazi duni ya Nairobi wajue kuwa Mungu anaweza kuwainua kuishi juu ya mazingira yao. Waombee wanaohudhuria vikundi vya maombi kwa siri, wakihofu kuwa waume wao wanaowanyanyasa watawapiga. Baadhi ya wanawake hawa walilazimishwa kuolewa na wanaweza kuuwawa wakijaribu kutoroka maana wahalifu ni wengi sana hapo wanakoishi.

**22** Ujumbe wa ukweli wa Biblia kufundishwa na wakristo waishi kulingana na neno la Mungu hata pale taratibu za kitamaduni zinakokubalika kwa kiwango kikubwa.

**23** Ulinzi wa wakimbizi na wakristo wapya walioacha tamaduni zao za dini ya asili; pia waombee waruhusiwe kuabudu kwa Uhurueneo la Afrika mashariki. Wakati huo huo, mtukuze Mungu kwa ajili ya uhuru wa kuabudu kwenye maeneo mengi ya Afrika mashariki bila hofu ya kisiasa au hofu za kidini.

**24** Viongozi wa Sudan kusini taifa jipya ulimwenguni wafanye kazi pamoja kuwalinda watu wote wanaotamani kuishi kwa amani na kuheshimiana. Ombea upatikanaji wa huduma za afya na watu wenye sifa zinazohitajika. Sudani kusini inahesabiwa kati ya nchi zenye idadi kubwa sana ya vifo vitokananvyo na uzazi *(http://www.unicef.org/southsudan/reallives_13025.html)*.

**25** Mwisho kwa utamaduni wa Sudan Kusini wa kuwauza mabinti ili kupata ng'ombe ("mahari). Baadhi ya wazazi huwasomesha wasichana si kwa manufaa yao bali waweze kudai ng'ombe nyingi wanapowauza kama bibi harusi *(http://www.internews.org/our-stories/project-updates/how-many-cows-for-educated-girl#sthash.CLDsdTYf.dpuf)*.

**26** Utoaji wa Mungu na hekima kwa ajili maendeleo ya huduma ya Project Hannah nchini Rwanda na kwa wanaoomba kwa kutumia kalenda za maombi zilizotafsiriwa kwa kifaransa na Kinyarwanda

**27** Gertrude anapoiongoza huduma ya Project Hannah nchini Uganda na kutembelea vikundi 11 makanisani na kwenye jamii. Ombea suluhisho za matatizo ya upungufu wa kompyuta na mtandao. Muombee John anapojitolea kutafsiri kalenda ya maombi kwa lugha ya Luganda kwa ajili ya waombaji.

**28** Wanawake wanaoishi na maambikizi ya VVU/UKIMWI. Wengi hudharauliwa na wenzi wao na ndugu wa familia na hawawezi kupata mahitaji yao muhimu. Waombee wanawake wazee wanaobeba majukumu mazito ya kutunza yatima ambao wazazi wao walifariki kutokana na maradhi yanayohusiana na UKIMWI.

**29** Watu wanaoishi kwa hofu kwenye maeneo ya vita Afrika mashariki waifahamu amani inayotoka kwa Bwana Yesu. "Na amani ya Mungu ipitayo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:7).


**30** Wanawake wanaoishi ndani ya tamaduni za kimila na kidini zenye athari hasi kwenye maisha yao na kuwazuia kupata uhuru ndani ya Kristo.

**Usikose kusikiliza kipindi cha *Wanawake wa matumaini* kwa siku na saa kama ifuatavyo:**

| | |
|---|---|
| • Kwa wakazi wa Moshi - Radio sauti ya Injili 96.2 FM : Siku ya Jumapili Saa 12:00 hadi saa 12:30 jioni. | • Kwa wakazi wa Dar es Salaam - Radio Wapo 98.1 FM: Siku ya Jumapili saa 9:30 hadi saa 10:00 mchana. |
| • Kwa wakazi wa Mwanza - Neema Radio – 98.2 FM : Siku ya Jumanne saa 2:00 Hadi saa 2:30 Usiku. | • Kwa wakazi wa Arusha - Radio safina 92.6 FM: Siku ya Jumapili saa 1:30 hadi saa 2:00 Usiku. |
| • Kwa wakazi wa Dodoma – Radio Uzima 94.0 FM Siku ya Jumatatu na Ijumaa Saa 2:30 hadi saa 3:00 Usiku. | • Kwa wakazi wa Zanzibar-Zenj Radio – 96.9 FM : Siku ya Jumanne saa 3:00 hadi saa 3:30 Usiku. |

**Kipindi cha *Wanawake wa Matumaini* kinarushwa kwa zaidi ya lugha 65. Kalenda maombi ya PH ya kila mwezi hutafsiriwa kwa zaidi ya lugha 80.**

# Kuombea *wanawake*



## Wa Afrika Mashariki

Burundi
Ethiopia
Kenya
Rwanda
Somalia
Sudan Kusini
Tanzania
Uganda

**Prayer Calendar September 2015**

***Swahili***

# SEPTEMBA 2015 • KUOMBEA WANAWAKE WA AFRIKA MASHARIKI
## (BURUNDI, ETHIOPIA, KENYA, RWANDA, SOMALIA, SUDAN KUSINI, TANZANIA, UGANDA)

Afrika Mashariki ni moja ya maeneo maskini sana duniani, na vurugu zilizopo Burundi pamoja na uhasama uliopo Somalia na Sudani kusini kwa muda mrefu unafanya maisha kuwa magumu kwa mamilioni ya watu. Ethiopia na Kenya zinatunza mamilini ya wakimbizi wanaotafuta usalama au walio kwenye hatari ya njaa. Wanawake wengi wa Afrika Mashariki wanakabiliana na changamoto zilizozoeleka za umaskini kupita kiasi, kutokujua kusoma, ndoa za lazima, ndoa za uke wenza, vurugu majumbani na matatizo ya kiafya kama vile ukeketwaji, kizazi kuachia, fistula, utapiamlo, vifo vitokananvyo na uzazi na UKIMWI.

Afrika Mashariki, wanawake hukutana makanisani kufanya maombi na pia kwenye nyumba zao. Nyumba zao nyingi ni ndogo, na wengi wao wana vitu vichache. Lakini hili hliwazuii wanawake hawa kuwaalika wengine nyumbani kwao kuomba au kuvisikiliza vipindi vya redio vya Wanawake wa matumaini. Wanawake wa Project Hannah pia hutoa fedha kwa ajili ya upasuaji na mahitaji mengine yanayowakabili wanawake kwenye jamii zao.

Marta anaongoza kipindi cha maombi cha Project Hannah. Hajawahi kwenda shule ila amejifunza kusoma Biblia na anafundisha kweli za Mungu kwa wanaomjia kupata ushauri maana aliwahi kuwa mkunga. Alipata matatizo ya kizazi kuporomoka kabla ya ukufanyiwa upasuaji. Anamtunza mume wake na watoto wake watano.

Durt alibaki mjane watoto wake wakiwa wadogo sana. Alipata watoto saba lakini watatu walifariki. Timu ya Project Hannah ilimuongoza kumjia Mungui na kumsaidia kupata matibabu kizazi chake kilipoporomoka.

Mume wa Workinesh alimfukuza yeye na watoto wake kutoka nyumbani kwao. Mahakama hazikumsaidia na kaka zake walimpiga kwa maana hawakutaka kushirikina naye kwenye mali za familia. Timu ya Project Hannah wamemnunulia godoro na sasa watoto wanalala kwenye chumba cha kupangisha.

## TAFADHALI OMBA KWA AJILI YA...

**1** Wanawake kujenga mahusiano mazuri na ndugu zao kwenye familia na pia na Mungu kupitia msaada wa vipindi vya redio vya Wanawake wa Matumaini. Pia mtukuze Mungu kwa maisha yaliyobadilishwa kupitia huduma za Project Hannah zinazowafikia wanawake kwa lugha zao wenyewe.

**2** Utulivu wa kisiasa na kiuchumu Afrika masharikí ili rasilmali zinazohitajika, matibabu na upatikanaji wa chakula uwepo kwa wanawake na familia zao. Ombea viongozi wafanye kazi pamoja kwa manufaa ya wananchi wao. Pia ombea wakimbizi na watu waliokosa makazi ndani ya nchi zao wanaotamani kupata mahali salama pa kuishi.

**3** Wanawake wanaojifungulia majumbani na wapo kwenye hatari ya kufa kutokana na matatizo yatokanayo na uzazi au mateso ya fistula kwa miaka mingi au vizazi kuachia baada ya uchungu pingamizi wa masaa mengi.

**4** Wanatimu wa Vipindi vya Wanawake wa matuiamini vya lugha za Amharic na Oromo (Hirut, Asrat, Woytu, Ayanitu, Genet, Yeshe, Alimazi, Yenalem, Gebayinesh, Galle, Zenebech, Berhane, Chalale, Agamitt, Yadatte, Dimuru, J alamme, Aregashe, Hadha, na Wawa Tisuga) wa Ethiopia ili familia zao ziwe na afya bora na imara. Waombee waweze kuwahudumia wasikilizaji wanaoishi kwa umaskini mkubwa, gerezani na wana matatizo makubwa ya afya (vizazi kuporomoka, fistula), wana madhara ya kunyanyaswa kama (Kumwagiwa tindikali, ndoa za utotoni, kubakwa).

**5** Wanawake wanaoteseka kwa vizazi kuporomoka. Wengi wao wametelekezwa na waume na wanahangaika kupata makazi na chakula kwa ajili ya watoto wao. Waombee wanawake wa Project Hannah Ethiopia wanaoonyesha upendo wa Kristo kwa wanawake hao kwa kuwalipia gharama za upasuaji unaohitajika, kuwapa chakula na nguo, kuwafanya marafiki na kushirikiana nao kwenye vikundi vya maombi na shughuli zingine.

**6** Uandaaji wa toleo la mwisho la kipindi cha igizo la redio cha Sauti ya Uponyaji na kwa ajili ya usambazaji na uenezaji salama kwa vyombo vyote vya habari huko Jinka, kusini mashariki mwa Ethiopia. Mtukuze Mungu kuwa uandaaji kwa lugha ya Ari umekamilika! Omba ili Sauti ya uponyaji kiwaelimishe wanawake wanaoteseka na fistula na kuwahakikishia upendo wa Mungu. Pia ombea mipango ya kurekodi kipindi cha Sauti ya uponyaji kwa lugha za Amharic na Oromo hivi karibuni.

**7** Wasichana wadogo wanaolazimika kukeketwa na kupata matatizo ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na maumivu makali kupita kiasi, kutokwa na damu hadi kuishiwa na maambukizo. Omba ili wazazi watambue kuwa vitendo hivu vyenye madhara vinatakiwa vikomeshe utamaduni huu. Kwa kuwa ukeketaji ni marufuku nchini Marekani na Uingereza, wasichana wengi wa kisomali hurudi barani Afrika ili kufanyiwa kitendo hiki..

**8** Uongozi na hekima kwa Timu za Project Hannah zinazoandaa vipindi kwa Kiswahili (Virginia, Lynn, Catherine, Linanh, Beverly, Elfriede, Mischnick, Winnie, Roselyn, na Christine) nchini Kenya na (Joyce, Agatha, Nen'ida, Msunza, Lilian, na Upendo Godwin) nchini Tanzania wanapotafsiri, kuweka kwenye mazingira halisi na kurekodi vipindi hivi ili wengi waguswe na kuongozwa kuwa na uhusiano binafsi na Mungu. Muombee pia Bernice (Mkurugenzi wa TWR Kenya).

**9** Wanawake wanaokabiliwa na vurugu za majumbani Afrika Mashariki. Mara nyingi polisi hupuuzia malalamiko na mashtaka huchukua miaka mingi hadi kufikishwa mahakamani. Nchini Kenya, madhara ya kubakwa na kujeruhiwa kimwili ni mambo ya kawaida na vitendo vya kunajisi na kubaka watoto vimeongezeka sana.

**10** Jitihada zaidi zifanyike kukomesha vitisho vya al-Shabab kaskazini mashariki nchini Kenya. Huduma nyingi za Wakristo na makanisa yamefungwa kutokana na vitisho vya kulipuliwa na kuuwawa. Ombea pia ulinzi wa Mungu kwa makanisa nchini Zanzibar na watu wanaokabiliwa na mateso.

**11** Ulinzi wa Mungu kwa watoto wake wanaokabiliwa na tabia mbaya za makundi rika na kusababisha wafanye maamzu yasiyokuwa sahihi maishani. Ombea walio kwenye hatari ya kutumia madawa ya kulevya, pombe na ibada za kishetani.

**12** Vikundi vya maombi vya Project Hannah nchini Kenya wapate mahali pa kukutania. Nyumba zao ni ndogo sana. Ombea pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ofisi na uchapaji na usambazaji wa kalenda nyingi zaidi kwa waombaji zaidi ya 2,000.

**13** Wanawake waliotelekezwa na waume zao au hawawaamini na kutunzwa na waume walio nao. Omba ili wanawake hawa wapate mafunzo ili waweze kuwatunza watoto wao. Ombea wajane na mama wanaowatunza watoto pekee yao wanaodharauliwa na wanahangaika ili kuweza kuishi.

**14** Nyumba ya Hannah nchini Tanzania, sehemu ya kuwafikisha huduma ya Project Hannah ambapo wanawake hujifunza kushona ili watoto wao wapate sare za shule na kutengeneza vitu vya kuwaingizia kipato. Ombea pia watu wenye moyo wa kujitolea wanaotoa fedha zinazohitajika kwa ajili ya usafiri kutembelea vikundi 175 vya maombi (zaidi ya waombaji 2,500) kutoka madhehebu 25 tofauti na mikoa 11 ya nchi nzima. Wanasafiri umbali mrefu wengine hadi masaa 19 kwa basi ili kuwafikia wasikilizaji na waombaji.

Project Hannah • P O Box 2426, Arusha, Tanzania • Simu: 075 494 5224 • info@phafrica.org • www.phafrica.org